


# Kurasimu Sheria Mama ya Nchi

## Tafakari za Wananchi wa Tanzania Bara kuhusu Rasimu ya Katiba






## 1. Utangulizi

Mnamo tarehe 3 Juni 2013, Tume ya Kukusanya Maoni ya Katiba (CRC) iliwasilisha Rasimu yake ya Katiba. Hatua hii ilichukuliwa baada ya kuwepo kwa maoni mengi yanayodai Katiba ya 1977 iundwe upya. Tangu kuzinduliwa kwa Rasimu hii ya Katiba, wananchi wa kawaida pamoja na wawakilishi wa makundi mbalimbali wamekuwa wakitoa maoni yao kuhusu Rasimu hiyo; hivyo, kuleta mjadala ulioshirikisha umma.

Muhtasari huu unawasilisha maoni ya hivi karibuni ya wananchi kuhusu Rasimu ya Katiba. Matokeo yamejikita katika awamu ya tano ya utafiti wa *Sauti za Wananchi*, ambao ni utafiti wa kwanza barani Afrika wenye uwakilishi wa nchi nzima unaofanyika kwa njia ya simu za mkononi (www.twaweza.org/sauti). Takwimu zilikusanywa kwa wahojiwa kutoka maeneo mbali mbali ya Tanzania *Bara*. Simu zote zilipigwa kati ya Julai 16 na Julai 30, 2013; Takwimu zinajumuisha maoni kutoka kaya 1,708.

Muhtasari huu unaelezea mambo muhimu yaliyogunduliwa yakiwemo yafuatayo:

- Asilimia 67 ya raia wa Tanzania Bara wanajua kuwaa Rasimu ya Katiba ilizinduliwa
- Asilimia 36 ya raia wa Tanzania Bara walishiriki katika mchakato wa kutoa maoni ya Katiba
- Asilimia 46 ya raia wa Tanzania Bara wako tayari kuunga mkono Rasimu ya Katiba kwa kura
- Asilimia 70 ya raia wa Tanzania Bara wangependa mawaziri wasiteuliwe kutokana na Bunge

Muhtasari huu umeandaliwa na Twaweza, iliyopo Hivos Tanzania. Wachangiaji ni Elvis Mushi, Youdi Schipper na Constantine Manda. Data zilikusanywa na Ipsos Tanzania. Umetolewa Novemba, 2013.

S.L.P. 38342, Dar es Salaam, Tanzania.
Simu: +255 22 266 4301.
uwazi@twaweza.org www.twaweza.org/sauti

Twaweza ni sisi


- Asilimia 65 ya raia wa Tanzania Bara wanaamini nchi itakuwa na Katiba mpya ifikapo 2015

# 2. Mambo saba kuhusu Rasimu ya Katiba

## Jambo la 1: Asilimia 48 wanaweza kueleza Katiba ni nini

Wananchi ni wanufaikaji wakuu wa Katiba kwa sababu Katiba ni chombo kinachofafanua uhusiano kati yao na muundo wa Serikali. Kutokana na hili, wananchi kuelewa Katiba ni jambo la muhimu sana. Hata hivyo, kama inavyoonyeshwa katika Kielelezo cha 1, asilimia 52 ya raia wa Tanzania Bara hawajawahi kusikia kuhusu Katiba au hawawezi kueleza Katiba ni nini. Pamoja na hayo, karibu nusu ya wahojiwa (48%) waliweza kutoa maelezo sahihi kuhusu lengo la Katiba.

**Kielezocha 1 : Je, unafahamu nini kushusu katiba?**





**Chanzo cha takwimu:** *Sauti za Wananchi,* Utafiti kwa Njia ya Simu ya Mkononi awamu ya 5, Julai 2013.

## Jambo la 2: Asilimia 29 walishiriki mikutano ya kuchangia maoni

Mikutano iliyoandaliwa na Tume ya Kukusanya Maoni ilifanikiwa kuwaleta pamoja karibu theluthi moja ya watu wote waliofikia umri wa utu uzima. Kama inavyoonyeshwa katika Kielelezo cha 2, wananchi wa Tanzania walishiriki katika mchakato wa kutoa maoni kupitia mikutano, kuandika maoni, kutuma ujumbe mfupi wa simu, mahojiano, baruapepe au vyombo vya habari vya kiraia (mtandaoni). Kwa kuhesabu wananchi wote walioshiriki kwa njia hizo, asilimia 36 ya raia wa Tanzania Bara walishiriki kwenye mchakato huu.

**Kielelezo cha 2: Ushiriki wa wananchi katika mchakato wa kutoa maoni ya Katiba**





**Chanzo cha takwimu:** *Sauti za Wananchi,* Utafiti kwa Njia ya Simu ya Mkononi awamu ya 5, Julai 2013.

## Jambo la 3: Asilimia 67 wanafahamu kuwa Rasimu ya Katiba imezinduliwa


Rasimu ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilizinduliwa na Tume ya Katiba katika viwanja vya Karimjee jijini Dar es Salaam, Tanzania tarehe 3 Juni, 2013. Mwezi mmoja na nusu baada ya uzinduzi huu, asilimia 67 ya wahojiwa walieleza kuwa wanafahamu kuhusu uzinduzi huo.

**Kielelezo cha 3: Uzinduzi wa Rasimu ya Katiba**

**Paneli ya A: Je, una habari kwamba serikali ya Tanzania hivi karibuni imezindua rasimu ya katiba?**




**Paneli ya B: Je, unajua wapi unaweza kupata nakala ya Rasimu ya katiba?**




**Chanzo cha takwimu:** *Sauti za Wananchi,* Utafiti kwa Njia ya Simu ya Mkononi awamu ya 5, Julai 2013.


Tume ya Katiba imefanya jitihada za kuhakikisha kuwa nakala za Rasimu ya Katiba, zilizochapwa na za kidijitali zinawafikia wananchi kwa urahisi. Kama kilelezo cha 3 (Jopo la B) kinavyoonyesha, asilimia 23 ya wananchi walijua wapi watapata nakala ya Rasimu.

## Jambo la 4: Asilimia 70 wangependa Baraza la Mawaziri lisitokane na Bunge

Rasimu ya Katiba ina vifungu 240 – karibu mara mbili ya vifungu vilivyokuwa katika Katiba ya mwaka 1977 – nyinginezo zikiwa ni "mada motomoto" ambazo zimekuwa zikijadiliwa mara kwa mara katika vyombo vya habari. Kielelezo cha 4 kinaorodhesha mambo kumi kati ya hayo na kutoa maoni na mapendekezo ya wananchi. Kutokana na takwimu hizi, inaonekana wananchi walio wengi wanakubaliana na mapendekezo mengi yaliyomo katika Rasimu hii ya Katiba.

Katika vipengele 10 ambavyo utafiti wa *Sauti za Wananchi* ulihoji, asilimia 91 ya wananchi walikubaliana na kipengele kilichomo kwenye Rasimu ya Katiba kinachowapa haki ya kuwaondoa wabunge madarakani iwapo watashindwa kutimiza wajibu wao ipasavyo majimboni. Hii ina maana kuwa wananchi wangependa kuwawajibisha wawakilishi wao. Kwa upande mwingine maoni yalitofautiana kuhusu pendekezo la kuwepo kwa serikali tatu.

**Kielelezo cha 4: Maoni ya Wananchi kuhusu mada zilizomo katika Rasimu ya Katiba**





**Chanzo cha takwimu:** *Sauti za Wananchi,* Utafiti kwa Njia ya SimuyaMkononi awamu ya 5, Julai 2013.

## Jambo la 5: Robo ya wananchi wangependa masuala ya Muungano yabaki kama yalivyo

Sauti za Wananchi ilitafuta kujua ni mabadiliko gani, kama yapo, ambayo wananchi wa Tanzania Bara wangependa yafanyike katika Muungano uliofanyika mwaka 1964 kati ya Tanganyika na Zanzibar. Swali lililotumika lilitokana na utafiti wa mwaka 2012 wa Afrobarometer (http://www.afrobarometer.org/). Majibu yaliyopatikana yalilinganishwa moja kwa moja na maoni ya mwaka uliopita. Zaidi, Afrobarometer 2012 ilijumuisha maoni ya wahojiwa kutoka Zanzibar.

**Kielelezo cha 5: Je, ungependa kuona mabadiko gani, kama yapo, yanafanywa kwenye Muungano wa mwaka 1964 kati ya Tanzania Bara "Tanganyika" na Zanzibar?**




**Chanzo cha takwimu:** *Sauti za Wananchi,* Utafiti kwa Njia ya Simu ya Mkononi awamu ya 5, Julai 2013 & Utafiti wa Afrobarometer, 2012

Kielelezo cha 5 kinalinganisha uungaji mkono wa miundo mbalimbali ya Muungano kama ilivyoripotiwa katika utafiti wa Afrobarometer (2012, Bara na Zanzibar) na ule wa *Sauti za Wananchi*. Kumbuka kuwa katika swali hili, wahojiwa walitakiwa kuwa na chaguo moja tu; ndiyo  maana wanaounga mkono muundo wa Serikali tatu wamepungua wakilinganishwa na wale wa Kielelezo cha 4 hapo awali.

Jambo la kushangaza katika matokeo ya utafiti wa *Sauti ya Wananchi* 2013 ni kiu kubwa ya kutaka mabadiliko ya Katiba miongoni mwa raia wa Bara: uungaji mkono kwa "hakuna mabadiliko" ni asilimia 26 ikilinganishwa na asilimia 47 ya mwaka 2012. Wakati huo huo, takwimu za utafiti wa *Sauti za Wananchi* zinaonyesha kwa kiasi gani  chaguo la "kuongezeka kwa madaraka zaidi kwa Zanzibar ndani ya Muungano" linazidi kuungwa mkono (32% ikilinganishwa na 8% katika utafiti wa Afrobarometer 2012). Hakuna maelezo rahisi na ya uhakika kuhusu nini kinasababisha tofauti hizi; mojawapo ya


sababu ni mijadala kupitia vyombo vya habari kuhusu Katiba, jambo ambalo limeokuza weledi miongoni mwa Watanzania na kuathiri maoni yao.

Pendekezo la Serikali tatu katika Rasimu ya Katiba linaungwa mkono sawa sawa na lile la muundo wa Serikali moja. Wahojiwa wengi zaidi wangependa kusiwe na mabadiliko yoyote katika muundo huu. Jambo linalovutia hisia, ni kuwa, wahojiwa walipoulizwa kuhusu maoni yao kila mmoja peke yake kuhusu chaguo la Serikali tatu  (tazama Jambo la 6 hapo juu), walionyesha kuunga mkono zaidi: asilimia 26 wakikubaliana sana na asilimia 25 wakilikubali kiasi.

## Jambo la 6: Zaidi ya nusu wangeunga mkono Rasimu ya Katiba

Rasimu mpya ya Katiba *haiwezi* kuwa sheria hadi ipigiwe kura na wananchi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ni lazima ipitishwe na wengi walau kwa nusu au zaidi (50% + 1 ya kura zote) kwa pande zote mbili (Bara na Zanzibar) ili iweze kuwa sheria mpya ya nchi.

**Kielelezo cha 6: Je, ungeiunga mkono Rasimu ya Katiba kwa njia ya kura au la?**





**Chanzo cha takwimu:** *Sauti za Wananchi,* Utafiti kwa Njia ya Simu ya Mkononi awamu ya 5, Julai 2013.

Kama inavyoonyeshwa katika Kielelezo cha 6, asilimia 46 ya wananchi wenye umri wa utu uzima wangepiga kura kupitisha Rasimu ya Katiba ya sasa; na asilimia 22 wangepiga kura kuipinga. Kwa maneno mengine,  hata kama wale ambao hawajaamua (asilimia 20) wangepiga, bado  zaidi ya nusu ya wapiga kura wa Tanzania Bara wangeiunga mkono Rasimu ya Katiba.

### Jambo la 7: Asilimia 65 wanaamini kuwa uchaguzi ujao utaendeshwa kwa kutumia Katiba mpya

Rasimu ya Katiba imependekeza mabadiliko kadhaa, mmojawapo ukiwa ni namna gani uchaguzi uendeshwe; na vile vile Serikali pamoja na Bunge vitumie muundo upi baada ya uchaguzi. Utafiti wa *Sauti za Wananchi* unaonyesha kuwa wananchi walio wengi (65%) wanatarajia Katiba Mpya itakuwa tayari wakati wa uchaguzi mkuu ujao wa 2015 (Kielelezo cha 7).

**Kielelezo cha 7: Je, unafikiri uchaguzi mkuu ujao utafanyika kwa kutumia Katiba ya sasa au Katiba Mpya?**




**Chanzo cha takwimu:** *Sauti za Wananchi,* Utafiti kwa Njia ya Simu ya Mkononi awamu ya 5, Julai 2013.

Kwa ufupi, pamoja na tofauti za maoni katika baadhi ya masuala ya Rasimu ya Katiba, watu wengi wana matumaini kuwa Katiba itapitishwa kabla ya uchaguzi mkuu wa 2015.

## 3. Hitimisho

Mjadala kuhusu Rasimu ya Katiba unaendelea nchini Tanzania. Kuna maswali kuhusu ni kwa kiasi gani Rasimu hii inaakisi maoni ya watu. Kutumia utafiti wetu *Sauti za Wananchi* wa kupitia njia ya simu za mkononi, kunaturuhusu kupata maoni ya wananchi kwa wakati halisi kuhusu suala hili na matukio mengine mengi. Utafiti huu ni wakilishi kwa Tanzania Bara, haihusishi Zanzibar.

Kwa kifupi, wananchi wa Tanzania Bara wana maoni yanayotofautiana kuhusu vipengele mbali mbali vya Rasimu ya Katiba, huku baadhi ya masuala yakiungwa mkono kuliko mengine. Idadi kubwa ya wananchi wanapinga wazo la kuteua mawaziri kutoka miongoni mwa Wabunge, kama utaratibu ulivyo hivi sasa. Suala la serikali tatu kwa kiasi kikubwa limefungamana ikiwa wanaounga mkono na wapingaji wakiwa wamegawanyika karibu asilimia 50-50. Masuala mawili yanaonekana wazi, kama rasimu ingekuwa imeshapigiwa kura hadi mwisho wa Julai 2013, wakati simu za *Sauti za Wananchi* zilipopigwa kwa

wahojiwa; na kama upigaji kura wenyewe ungefuata mapendekezo hayo yaliyosemwa, Rasimu ya Katiba ya sasa ingepata kura za kutosha kutoka Tanzania Bara.

Ni jambo muhimu kuakisi maoni ya wananchi yanavyobadilika kuhusiana na suala ka Katiba, kama *Sauti za Wananchi* walivyofanya kwa kulinganisha matokeo haya na yale ya utafiti wa Afrobarometer uliofanyika mwaka mmoja uliopita. Hatuwezi kusema kwa uhakika kabisa kuwa Rasimu ya Katiba itapita; lakini inadhaniwa kuwa matokeo haya yatachangia katika mjadala wa umma kadiri mchakato unavyoendelea kuelekea kwenye kura ya maoni.